

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



## TAARIFA KWA UMMA

### **Kufunguliwa Dirisha la Udahili Awamu ya Nne**

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inawatangazia umma kuwa maombi ya udahili kwa awamu ya nne kwa mwaka wa masomo 2018/2019 yatafunguliwa kuanzia tarehe 13.10.2018 hadi tarehe 20.10.2018.

Waombaji wapya na wale ambao hawakuchaguliwa katika awamu zilizopita wanahimizwa kutumia fursa hii ya mwisho kutuma maombi yao ya udahili moja kwa moja kwenye Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu nchini.

**Waombaji wote wanakumbushwa kuomba programu ambazo wanakidhi vigezo kama ilivyoelekezwa katika Kitabu cha Mwongozo wa Udahili (Admission Guidebook).**

**NB: Tume inaelekeza Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu kutangaza programu ambazo bado zina nafasi na idadi ya nafasi zilizobaki ili waombaji waweze kutuma maombi yao.**

**Imetolewa na:**

**Katibu Mtendaji  
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania  
12/10/2018.**